TANGAZO LA KAZI ZA WADADISI KATIKA WILAYA YA KYELA

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU (NBS) INAWATANGAZIA WATANZANIA WENYE SIFA ZILIZO HAINISHWA HAPA CHINI KUWASILISHA MAOMBI YA KAZI MUDA YA UKUSANYAJI WA TAKWIMU/ UDADISI KWAJILI YA UTAFITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI KWA MWAKA 2017/2018. MWOMBAJI ANATAKIWA ATOKEE KWENYE ENEO AMBALO UTAFITI UNAFANYIKA MAENEO HAYO NI :-

KATA YA MBUGANI, KATA YA KATUMBASONGWE (TEMEKE), KATA YA IPINDA (MABUNGA), KATA YA MATEMA/MABABU (NKESO B).

a. SIFA ZA MSINGI ZA MWOMBAJI

i. Umri wa miaka 18 na kuendelea

ii. Elimu ya kuanzia kidato cha nne

iii. Mkazi wa eneo lililochaguliwa kwajili ya utafiti na awe tayari kufanya kazi kwa kipindi chote cha miezi kumi na mbili

b. SIFA ZA ZIADA ZA MWOMBAJI

i. Elimu ya cheti cha ukusanyaji wa takwimu rasmi kutoka Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika

ii. Uzoefu wa kazi ya ukusanyaji takwimu katika tafiti mbalimbali za NBS

iii. Uwezo wa kutumia tablets na CAPI wakati wa ukusanyaji takwimu

Aidha mwombaji anatakiwa kuandika barua kwa mkono akionesha anuani kamili na namba yake ya simu na kuambatanisha nakala ya vyeti vyote vya elimu na mafunzo, CV,Barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji wa kijiji ambacho utafiti unafanyika na picha mbili zilizopigwa hivi karibuni. Maombi yatumwe kabla ya tarehe 12.08.2017 kupitia anuani ifuatayo:

Meneja Takwimu wa Mkoa,
Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
S.L.P 841,
Mbeya.